hayo, naendelea kwa aliyeko hadi mwisho na ikibainika

ngwa na wakili Faudhia Mustapher anayemtetea Sabaya,

wao kama muongozo ya kisheria inavyoelekeza.

HABARI LEO UK 7

# * Ataja mikakati kuimarisha sekta ya uvuvi Ziwa Victoria *

**Na Nashon Kennedy, Mwanza**

IMEELEZWA kuwa sekta ya uvuvi kwa ukanda wa Ziwa Victoria inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo ya utoroshaji wa mazao ya samaki kwa njia ya maji unaofanywa visiwani kwa kutumia mipaka isiyo rasmi na bila kupitia kwenye masoko yaliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria.

Hayo yalielezwa juzi kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) na Ofisa Uvuvi wa Mkoa wa Mwanza, Titus Kilo alipokuwa akiwasilisha taarifa ya maendeleo ya sekta ya uvuvi na mikakati ya kuboresha sekta hiyo.

Alizitaja sababu zingine kuwa ni kupungua kwa upatikanaji wa samaki kwenye viwanda vya kuchakata minofu ya samaki, uhaba wa uchakavu wa vitendea kazi kama pikipiki, magari na boti na upungufu wa watumishi.

"Watoroshaji hudanganya kwa kutumia vibali vya ndani wakati wanasafirisha samaki hao kwenda nje ya nchi," alisema na kuzitaja sababu zingine kuwa ni uhaba wa upatikanaji wa chakula cha samaki ikiwemo bei kubwa ya samaki.

Aliitaja mikakati iliyowekwa na mkoa kwa ajili ya utatuzi wa changamoto hizo kuwa ni kuimarisha ulinzi na usimamizi wa mazalia ya samaki ili kuongeza uzalishaji wa samaki majini ambao kwa sasa unatishiwa na vitendo vya uvuvi haramu.

"Mkakati mwingine ni kuongeza nguvu kwenye ufugaji wa samaki kwenye vizimba na mabwawa ili kusaidia kukidhi mahitaji ya soko la ndani," alisema.

Alisema mkakati mwingine ni kufanya udhibiti kwenye maeneo ya kimkakati yaliyoko ziwani na mipakani ili kuwafanya wafanyabiashara wote kufanya biashara ya samaki ndani na nje ya nchi kwa kufuata taratibu za sheria na biashara ya uvuvi.

"Mkakati mwingine ni kuendelea kuhimiza wawekezaji kujenga kiwanda cha kuzalisha chakula cha samaki kanda ya ziwa", alisema na kuongeza kuwa mkakati mwingine ni serikali kuendelea kuondoa tozo kwa chakula cha samaki kinachoagizwa kutoka nje ya nchi na kuajiri watumishi wapya.

CamScanner

# Migogoro wakulima, wafugaji janga linalohitaji kukoma sasa

**Na Sabato Kasika**

MIGOGORO ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji imekuwa ikijirudia kila mwaka na kusababisha baadhi ya mali za watu kuharibiwa, kuumizana na hata wakati mwingine kuwapo kwa umawagaji damu.

Hayo yote yanatokana na kutokuwapo kwa maeneo maalum kwa ajili ya shughuli za ufugaji na kusababisha mifugo kuingia kwenye maeneo ya wakulima kitendo ambacho huzusha migogoro hiyo.

Wapo baadhi ya wakulima ambao wamewahi kufikia hatua ya kukata mifugo kwa mapanga, kama njia ya kulipiza kisasi baada ya wafugaji kuingiza mifugo hiyo katika mashamba ya wakulima na kusababisha uharibifu.

Wakati tunaelekea kuhitimisha mwaka 2022, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, amekutana na viongozi wa serikali ya mkoani Morogoro katika kikao kilichotokana na maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, yanayohusu kusimamia kwa karibu sekta ya mifugo, ili kutatua changamoto hizo.

Pamoja na mengi ambayo Waziri Mkuu aliongea katika kikao hicho, inasikitisha kusikia kuwa kumekuwapo na vitendo vya rushwa miongoni mwa viongozi ambao pia wamekuwa wakichochea migogoro hiyo.

Lakini akafafanua kuwa polisi wenyewe sasa hivi wameanza kudhibitiwa na wananchi na kwamba ikifikia hapo hiyo haina tija, chombo cha ulinzi na usalama kinadhibitiwa na raia.

Ninadhani inapofikia hapo, ina maana kuna jambo haliko sawa kama alivyosema Waziri Mkuu kuhusu rushwa miongoni mwa viongozi wanaopewa chochote na kuruhusu wafugaji kuingia katika maeneo yasiyoruhusiwa.

Kwa mtindo huo, ni wazi migogoro ya ardhi inayosababisha uhasama kati ya wafugaji na wakulima haitakwisha, hivyo ingependekeza viongozi wanaoamini kuwa kauli ya Waziri Mkuu imewagusa, basi wabadilike.

Mwaka 2023 uwe ni wa kuanza ukurasa mpya wa kuelewana na kuishi kama ndugu, badala ya uhasana unaosababishwa na migogoro ya ardhi. Utashi wa kisiasa unaotumiwa na serikali upewe nafasi kumaliza migogoro hiyo.

Ikumbukwe kwamba, mikoa 11 ya Morogoro, Iringa, Pwani, Lindi, Arusha, Manyara, Kagera, Katavi, Tabora, Tanga na Mwanza inatajwa kuongoza katika migogoro hiyo. Ingependeza kama haitaongezeka.

Njia nzuri ya kuifanya mikoa isiongezeke au migogoro iishe kabisa, ni kila kiongozi kuwajibika kwa kusimamia haki, usalama na kutoa elimu kwa jamii ambayo kwa sasa imekuwa na roho ya kikatili.

Kwa mujibu wa ripoti ya Global Peace Index (GPI) inayotolewa na taasisi ya uchumi na amani (IEP) yenye makao yake makuu mjini Sydney nchini Australia, Tanzania inaongoza kwa amani Afrika Mashariki.

Tanzania imeshika nafasi ya saba 7 kwa kuwa nchi yenye amani kwa nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara na duniani, ikiwa imeshuka kutoka nafasi ya 51 mwaka 2018 hadi nafasi ya 54 mwaka 2019 kati ya nchi 163.

Ni vyema amani hiyo isivurugwe na watu wachache wanaopenda rushwa na kusababisha wakulima na wafugaji ambao kwa miaka mingi wamekuwa wakiishi pamoja bila ugomvi hado miaka ya hivi karibuni.

Kimsingi, mkuu wa nchi anapoonyesha kutoridhishwa na maeneo fulani, ni wajibu wa viongozi au wasaidizi wake kuweka mipango ambayo itasaidia kudhibiti viashiria vyote vya uvunjifu wa amani kati ya makundi hayo mawili.



Baadhi ya wafugaji waliovamia Hifadhi ya Bonde la Mto Kilombero. **PICHA: MAKTABA**

> Ninadhani inapofikia hapo, ina maana kuna jambo haliko sawa kama alivyosema Waziri Mkuu kuhusu rushwa miongoni mwa viongozi wanaopewa chochote na kuruhusu wafugaji kuingia...

Leo migogoro ya ardhi inatajwa kushamiri kwenye mikoa 11, lakini ninaamini kuwa inaweza kupanuka hadi mikoa mingine iwapo hakutakuwa na mipango madhubuti ya kudhibiti viashiria hivyo mapema.

Kauli ya Waziri Mkuu itoshe kuwashtua viongozi ambao wanatajwa kujihusisha na rushwa na kuruhusu mifugo kuingia katika maeneo ambayo hairuhusiwi kuingia au kuvamia mashamba ya wakulima.

## MAAGIZO YA RAIS

Katika hotuba yake baada ya kulifunga rasmi geti la handaki lililojengwa kuchepusha maji, ili kupisha ujenzi wa bwawa la Nyerere lililoko Rufiji mkoani Pwani, aliagiza kushughulikiwa kwa familia 12 za viongozi waliovamia na kuchepusha maji Bonde la Ihefu.

Rais Samia aliwaagiza wakuu wa mikoa na wilaya kuondoa mifugo yote iliyoingizwa katika Bonde la Ihefu kinyume na utaratibu na kwamba ile itakayohamia maeneo ya vijiji katika bonde hilo, uwezo wa vijiji utaangaliwa.

Rais Samia pia aliagiza kwamba, wanaposhughulikia migogoro hiyo, wakafanye kazi zao kwa mujibu sheria kwa kuzingatia weledi na haki za binadamu.

"Tuna uzoefu wa mapigano ya wakulima na wafugaji hasa mkoani Morogoro na katika wilaya moja nadhani Kilosa mkuu wa wilaya alipoulizwa kwa nini wako wengi wanakufa kutokana na haya mapigano jibu lake ng'ombe wengi ni wa wakubwa nashindwa kuwagusa sasa niwaambie hakuna mkubwa atakayetuharibia mradi huu," Rais.

Rais anaagiza wakuu wa wilaya na mkoa wakafanye kazi na kwamba watakaoogopa wakubwa waseme washughulikiwe. Wale wanaochepusha maji wazuiwe Mto Rufiji ili maji yapite mkondo wake wa asili.

HATUA>> Zinapaswa kuchuchukuliwa

**UHURU**

MAONI YA MHARIRI

# Juhudi bado zahitajika kukomesha migogoro ya wakulima, wafugaji

KATIKA gazeti la **Uhuru** toleo letu la jana, tulichapisha habari inayohusu wakulima wilayani Kilosa, mkoani Morogoro kuchapwa viboko na kundi la watu wanaodaiwa jamii ya wafugaji.

Vurugu hizo zilitokea, zikiwa zimepita siku kadhaa tangu Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akemee na kuagiza kushughulikiwa kwa matukio ya namna hiyo miongoni mwa jamii.

Pia, Rais Dk. Samia aliitaka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kubuni mipango ya ufugaji wa kisasa huku akiwataka wakuu wa wilaya kusimamia sheria katika udhibiti wa mifugo katika vyanzo vya maji na uharibifu wa mazingira.

Rais Dk. Samia alitoa agizo hilo, alipohutubia Watanzania, akizindua ujazaji wa maji katika Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere, kwamba migogoro ya wakulima na wafugaji wilayani Kilosa ishughulikiwe.

Alisema hatua zinapaswa kuchukuliwa kwa sababu hakuna mtu aliye juu ya sheria.

Hata hivyo, tunasema kujitokeza kwa tukio la juzi la wakulima kuchapwa viboko ni jambo linalopaswa kuchukuliwa hatua za haraka kabla hali haijawa tete kati ya wafugaji na wakulima.

Hii inatokana na tukio la juzi lililotokea katika Kijiji cha Mvumi, wilayani Kilosa, ni kama vile agizo la Rais Dk. Samia halijasimamiwa vyema ndio maana kumeanza kujitokeza matukio hayo ya uvunjifu wa amani.

Tunaamini chanzo kikuu cha migogoro ya wakulima na wafugaji ni kutokuwa na maeneo maalumu kwa shughuli za ufugaji ndio maana wakati mwingine mifugo huingia katika maeneo ya wakulima na kula mazao mbalimbali na kusababisha hasara kubwa.

Pamoja na hayo, tunaamini huu ni wakati mwafaka kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kubuni mikakati ya kisasa kuhakikisha ufugaji unakuwa ajenda ya taifa na kuhakikisha uwepo wa maeneo maalumu ya ufugaji ambayo mahususi kwa malisho.

Kufanya hivyo itasaidia kuondoa migogoro isiyokoma kati ya wakulima na wafugaji na udhibiti wa uharibifu wa mazingira maeneo mbalimbali ya nchi kutokana na shughuli za binadamu ikiwemo mifugo.

Utamaduni mbovu uliopo wa kila mtu kufuga au kulima katika vyanzo vya maji ni jambo linalopaswa kuchukuliwa hatua za haraka kuondoa migogoro isiyokuwa na sababu za msingi.

Pia, wakati umefika kwa wakuu wa mikoa na wilaya kusimama imara na kukemea viashiria vyote vya uvunjifu wa amani kati ya wakulima na wafugaji ikiwemo kuwachukulia hatua kali za kisheria wanaofanya makosa ya makusudi.

Hakika kuadhibiwa kwa kundi korofi itafanya kuwepo utulivu na amani ambayo mara kwa mara imekuwa ikitoweka kutokana na ukaidi wa upande mmoja au makundi yote kwa ujumla wake.

Tunatoa rai kwa viongozi kusimamia kwa ukamilifu maagizo yanayotolewa kuondoa changamoto zilizopo, ambazo zimekuwa na athari kubwa kwa jamii.